

# MFUKO WA TAIFA WA BIMA YA AFYA

**Simu:** +255-22-2133964,  
2133969, 0800 110063  
**Barua Pepe:** info@nhif.or.tz  
**Tovuti:** [www.nhif.or.tz](http://www.nhif.or.tz)  
**Nukushi:** +255-22-2133972,  
2133982



**Makao Makuu**  
**Kurasini Bendera Tatu**  
**S.L.P. 11360, Dar es Salaam**  
**Tanzania**

## TAARIFA KWA UMMA

### ZOEZI LA UHAKIKI WA WANACHAMA WASTAAFU WA NHIF

Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) unawataarifu Wanachama wake waliosajiliwa kwa utaratibu wa Wastaafu kuwa kutakuwa na zoezi la uhakiki uanachama wao kwa kusudi la kuhisha taarifa za uanachama na kuweka kumbukumbu sahihi. Taarifa za uhakiki huu ni kama ifuatavyo:-

- i. Uhakiki utawahusu wanachama wastaafu walioandikishwa katika Mfuko kuanzia mwezi Julai 2009 hadi kufikia Septemba 2018.
- ii. Uhakiki huu utafanyika kwa miezi mitatu kuanzia **tarehe 1 Januari hadi 30 Machi 2019** katika Ofisi zote za NHIF zilizopo mikoa yote ya Tanzania Bara na Ofisi ya Zanzibar.
- iii. Mwanachama mstaafu atahitajika kufika katika ofisi yoyote ya NHIF akiambatana na mwenza wake (endapo yupo). Endapo mwanachama mstaafu amefariki, mweza aliyebaki atatakiwa kufika kwa ajili ya uhakiki.
- iv. Atatakiwa kufika na vitu vifuatavyo kwenye uhakiki:-
  - Vitambulisho vya NHIF
  - Cheti cha ndoa (kwa Mstaafu mwenye mwenza)
  - Kitambulisho cha Uraia **au** Mpiga kura **au** Leseni ya gari **au** Hati ya kusafiria.

Aidha, Mfuko unapenda kuwahimiza wanachama wastaafu kuzingatia tangazo hili na muda uliowekwa ili kuepuka usumbufu wa kukosa huduma kwa kutokufanya hivyo.

Kwa mawasiliano zaidi tafadhali piga simu huduma kwa wateja 0800 110063

**“Huduma Bora za Matibabu ni Haki yako na ni Dhama yetu”**

Imetolewa na;

**OFISI YA MAHUSIANO**

**DESEMBA 4, 2018**